# Kuelewa Mahudhurio ya Shule: Ufunguo wa Kufaulu katika Masomo

Watoto wanaohudhuria shule mara nyingi wana uwezekano mkubwa wa kufanya vizuri shuleni. Wanafunzi wanaohudhuria shule kila siku wana uwezekano mkubwa mara tisa zaidi wa kuhitimu kutoka shule ya upili. Pia wana uwezekano mkubwa mara sita zaidi wa kufaulu katika kusoma wafikapo katika darasa la tatu. Kwa sababu hii, watoto wanatarajiwa kuhudhuria shule mara nyingi kadri iwezekanavyo. Katika jimbo la Ohio, shule huweka kumbukumbu ya idadi ya saa ambazo watoto wamehudhuria shule.

## Watoto ambao huhudhuria shule mara kwa mara:

- Hupata alama bora zaidi. Hujifunza Kiingereza haraka zaidi.
- Hujisikia vizuri kuhusu wao wenyewe. Hufurahia shule zaidi.
- Huwa na uhusiano mzuri na wanafunzi wenzao na walimu.

## Je, unapaswa kufanya nini wakati mtoto wako anahitaji kukosa kuhudhuria shule?

Wasiliana na shule ili useme kwamba hatakuwepo shuleni. Unaweza kupigia simu ofisi ya shule ili uwajulishe kuwa mtoto wako hatakuwepo shuleni.

> Jambo hili ni muhimu. Sheria ya jimbo inahitaji shule ziwasiliane na familia za wanafunzi ambao hawapo shuleni ndani ya saa mbili baada ya kuanza kwa siku ya masomo. Shule nyingi hutumia simu za kiotomatiki kuwasiliana na wazazi ikiwa mwanafunzi hakuomba ruhusa ya kutokuwepo shuleni. Shule nyingi zina nambari tofauti ya simu ya mahudhurio ya kusema kuwa mwanafunzi hajahudhuria shule.
>
> Sheria hii inatumika ili familia na shule zijue mahali ambapo watoto wapo na kwamba wako salama.

Mtoto wako anaporudi shuleni patia shule barua inayoelezea kwa nini mtoto wako hakuwepo shuleni. Ikiwa uliomba ruhusa ya kutokuwepo shuleni, hakikisha kuwa

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

unatoa nyaraka au nyenzo zozote ambazo shule huomba. Barua ya daktari ni mfano wa kawaida. Wakati mwingine shule haitachukulia kuwa uliomba ruhusa ya kutokuwepo shuleni. Jambo hili hutokea familia zinapokosa kutoa barua au nyenzo nyingine zinazohitajika na shule.

> Unaweza kuomba barua. Uliza, "Naomba unipe barua ya ruhusa ya kutokuwepo shuleni ili mtoto wangu aipeleke shuleni."

Waulize walimu wa watoto wako. Angalia ikiwa kuna kazi yoyote au nyenzo zozote ambazo mtoto wako anapaswa kupitia. Hasa ikiwa mtoto wako anakosa kuhudhuria shule kwa siku nyingi za maosmo.

> "Je, mtoto wangu anaweza kufanya nini ili ajifunze masomo na kazi alizokosa?"

## Je, mahudhurio mazuri ni nini?

Wanafunzi wanapaswa kuhudhuria shule mara nyingi kadri inavyowezekana. Mara nyingi, kuchelewa kufika shuleni kunaweza kuathiri vibaya mafundisho ya mtoto wako jinsi ambavyo kukosa kuhudhuria shule kwa siku nyingi huathiri masomo. Wanafunzi wanapokosa kuhudhuria shule, wanakosa mafundisho. Wanaweza kukosa mafundisho ambayo wanafunzi wenzao wamepata haraka. Shule hujali mafanikio ya wanafunzi. Huwa zinachukua hatua za ziada ili ziwasaidie wanafunzi wanaohitaji msaada wa kufika shuleni.

Kuna aina mbili za kutokuwepo shuleni: kutokuwepo shuleni kwa ruhusa na bila ruhusa. Aina ya kutokuwepo shuleni huwa tofauti katika shule mbalimbali, kwa hivyo ni muhimu kujua kanuni maalum za shule yako mwenyewe. Kwa mfano, ikiwa unahitaji kuhudhuria miadi ya kisheria au kumpeleka mtoto wako kwa daktari, shule inaweza kuchukulia kuwa mwanafunzi hakuwepo shuleni kwa ruhusa. Ili upate ruhusa ya mtoto wako kutokuwepo shuleni, huenda ukahitaji kuonyesha barua kutoka kwa daktari, wakili, au mtu anayeweza kuthibitisha sababu yake ya kutokuwepo shuleni. Ukifanya hivyo, shule itaelewa kuwa alihitaji kutokuwepo shuleni, na haitaandika kuwa hakuwepo shuleni siku hiyo katika kumbukumbu ya mahudhurio ya mtoto wako.

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 

## Je, mambo gani hutokea wanafunzi wanapokosa kuhudhuria shule kwa siku nyingi?

Watoto wanapokosa kuhudhuria shule kwa siku nyingi, wanakosa muda wao mwingi wa kujifunza na wanaweza kukosa mafundisho ambayo wenzao walipata haraka. Hii ndio sababu shule hufuatilia mahudhurio ya kila mwanafunzi.

### Mambo ambayo shule inaweza kufanya:

- Kuwasiliana na familia yako ili kukujulisha kuhusu kutokuwepo kwa mtoto wako shuleni na kuhakikisha kuwa mtoto wako yuko salama.
- Kutuma barua nyumbani. Barua hii inapaswa kutumwa ikiwa imeandikwa katika lugha unayopendelea kutumia. Ulipomwandikisha mtoto wako shuleni, walipaswa kukuuliza kuhusu lugha unayopendelea kutumia. Ukibadilisha lugha unayopendelea kutumia, unaweza kuomba shule isasishe au ibadilishe taarifa hiyo.
- Kumtuma mtu nyumbani kwako ili ahakikishe kuwa mtoto wako yuko salama.
- Kuwasiliana na familia yako ili kuunda mpango wa kuhakikisha kuwa mtoto wako anahudhuria shule mara kwa mara.
- Kuuliza kuhusu usaidizi ambao familia yako inahitaji.
- Kutoa huduma za kumsaidia mtoto wako kuhudhuria shule kila siku.

### Familia yangu inaweza kufanya nini:

Unaweza kupigia shule simu ili ujue machaguo yanayopatikana. Unaweza kuzungumza na afisa wa mahudhurio, mwalimu mkuu, au mfanyakazi yeyote wa shule. Unaweza kueleza kwa nini mtoto wako huwa anakosa kuhudhuria shule. Mara nyingi, shule inaweza kusaidia familia kama yako kuhakikisha kuwa mtoto wako anafika shuleni kwa wakati unaofaa kila siku.

## Maswali Unayoweza Kuuliza

- Je, ninapaswa kufanya nini mtoto wangu akikosa kuhudhuria shule?
- Je, ninapaswa kufanya nini ikiwa mtoto wangu anahitaji kutokuwepo shuleni kwa ajili ya likizo ya kitamaduni au ya kidini? Je, ninaweza kufanya nini ikiwa sina njia ya kumpeleka mtoto wangu shuleni?

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

- Je, nnaweza kufanya nini ikiwa siwezi kumchukua mtoto wangu kutoka shuleni?
- Mtoto wangu huwa anakataa kwenda shuleni na hataki kuniambia sababu ya kukataa. Je, nifanye nini? Je, ninaweza kumwomba nani msaada? Nilipokea barua ya posta kuhusu mahudhurio ya mtoto wangu. Je, kuna mtu ninayeweza kuzungumza naye kuhusu jambo hili?

## Vidokezo vya Kumsaidia Mtoto Wako kuwa na Mahudhurio Mazuri

- ☐ **Jaribu kuelewa kwa nini mtoto wako hataki kwenda shuleni.** Wakati mwingine huenda mtoto wako hataki kwenda shuleni. Jambo hili likitokea, zingatia kuelewa jinsi mtoto wako anavyohisi na kwa nini hataki kwenda shuleni. Hakikisha kuwa unashughulikia masuala au wasiwasi wake.
- ☐ **Ikiwa mtoto wako huwa anakataa kwenda shuleni mara nyingi na hawezi kukuambia sababu ya kukataa, panga miadi na mwalimu au mshauri nasaha wa shule.** Wanaweza kukusaidia kujua kwa nini mtoto wako huwa hataki kwenda shuleni.
- ☐ **Punguza muda ambao mtoto wako hukosa kuhudhuria shule kwa ajili ya miadi ya matibabu au ugonjwa.** Ikiwa unaweza, panga miadi katika siku isiyo ya masomo au wakati wa mapumziko. Mruhusu tu mtoto wako akae nyumbani wakati anaumwa kweli au ikiwa ana ugonjwa wa kuambukiza. Angalia mfano huu wa barua ambayo unaweza kutumia kusema kwamba mtoto wako hatakuwepo shuleni.
- ☐ **Msaidie mtoto wako kuwa na afya njema ili aweze kuepuka kuwa mgonjwa na kukosa kuhudhuria shule.** Njia moja ambayo anaweza kuwa na afya njema ni kuhakikisha kuwa mtoto wako anakula chakula chenye lishe bora chenye matunda mengi na mboga na ana fursa za kufanya mazoezi kila siku kupitia timu ya michezo au wakati wa kucheza nje.
- ☐ **Panga matukio ya familia ukizingatia ratiba ya shule ya mtoto wako.** Panga safari za familia na sherehe wakati wa likizo ya shule au katika siku za wikendi.
- ☐ **Zungumza na mwalimu wa mtoto wako au shule haraka iwezekanavyo.** Ni muhimu kujulisha mwalimu au shule kukiwa na dharura za familia au safari

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

ambazo hazikutarajiwa. Mwalimu atakusaidia kuamua ikiwa mtoto wako anaweza kufanya kazi zake mapema au ikiwa mtoto wako anaweza kuchukua kazi ambayo anaweza kukamilisha anapokuwa mbali na shule.

- **Jitayarishe mapema.** Msaidie mtoto wako kujiandaa kwa ajili ya shule kwa kupanga nguo au vitu atakavyohitaji shuleni katika siku inayofuata kila usiku. Weka kitu kingine chochote ambacho atahitaji katika siku inayofuata mahali ambapo wewe au mtoto wako mnaweza kukipata kwa urahisi.
- **Hakikisha kuwa mtoto wako anapata usingizi wa kutosha.** Hakikisha kuwa mtoto wako anapata usingizi wa kutosha, takriban saa 8 hadi 12. Kupata usingizi wa kutosha husaidia watoto kuamka kwa wakati unaofaa na kuhisi kuwa hawajachoka na kuwa wako tayari kwa siku inayofuata. Mtoto wako anapaswa kupumzika kabla ya wakati wa kulala kwa kufanya shughuli isiyohusu kelele, kama vile kusoma badala ya kutazama televisheni au kutumia simu ya mkononi!
- **Omba huduma ya mkalimani.** Unaposhirikiana na shule, ijulishe shule ikiwa ungependa kuwa na mkalimani au kuzungumza na mtu ambaye anaelewa lugha na utamaduni wako. Unaweza pia kuomba shule ikutumie vijitabu vya maelekezo au taarifa iliyotafsiriwa kwa lugha unayopendelea.

Jifunze zaidi kuhusu kumsaidia mtoto wako kuwa na mahudhurio mazuri kwenye ukurasa wa Mahudhurio wa Colorin Colorado's School.

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

## Mfano wa Barua ya Kutuma Shuleni

Hapa kuna mfano wa barua au ujumbe wa kutuma shuleni wakati mtoto wako anakosa kuhudhuria shule. Unaweza kutumia mfano huu kuandika barua kwa mkono au kuutumia kutuma ujumbe mfupi au barua pepe kwa walimu au shule ya mtoto wako. Unachohitaji kufanya ni kuongeza taarifa yako.

Mpendwa {andika jina la mfanyakazi wa shule},

Tafadhali msamehe mtoto wangu {andika jina la mtoto wako} kwa kutokuwepo shuleni mnano tarehe {andika tarehe ambayo mtoto mtoto alikosa kuhudhuria shule} kwa sababu {andika kwa nini mtoto wako alikosa kuhudhuria shule}. Unaweza kuwasiliana nami kwa {andika nambari yako ya simu, barua pepe, au njia bora zaidi ambayo shule inaweza kutumia kuwasiliana nawe} ikiwa unahitaji taarifa zaidi kutoka kwangu.

Asante,

{Tia saini ya jina lako hapa}

## Sample Note to Send to School

Dear {andika jina la mfanyakazi wa shule},

Please excuse my child {andika jina la mtoto wako} for missing school on {andika tarehe ambayo mtoto mtoto alikosa kuhudhuria shule} because { andika kwa nini mtoto wako alikosa kuhudhuria shule}. You can contact me at {andika nambari yako ya simu, barua pepe, au njia bora zaidi ambayo shule inaweza kutumia kuwasiliana nawe} if you need more information from me.

Thank you,

{Tia saini ya jina lako hapa}

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

## Rasilimali za Ziada

- Unaweza kujifunza zaidi kutoka katika sehemu ya Mahudhurio ya Zana ya Familia ya NCELA unapochagua Sura ya 2. Inapatikana katika lugha nne (Kiingereza, Kiarabu, Kichina, na Kihispania). https://ncela.ed.gov/educator-msaada / vifaa / familia-toolkit
- Ukurasa wa Ufunguo wa Kufaulu Shuleni wa Colorin Colorado School hutoa vidokezo kuhusu mahudhurio. https://www.colorincolorado.org/article/school-attendance-key-success
- Mpango wa Attendance Works hutoa vijitabu vya maelekezo kuhusu mahudhurio katika madarasa tofauti vinavyopatikana katika lugha nyingi. https://www.attendanceworks.org/resources/handouts-for-families
- Mpango wa Attendance Works pia hutoa vidokezo kwa familia unapoamua ikiwa mtoto wako ni mgonjwa na anahitaji kukaa nyumbani na kutokuwepo shuleni. https://www.attendanceworks.org/resources/handouts-for-families
- Pata vidokezo vya mahudhurio kwa familia kwenye tovuti ya shule za umma za Albuquerque. https://www.aps.edu/news/archives/news-from-2021-2022/attendance-tips-for-families

*Rasilimali hizi zinalenga kuimarisha masomo, ustawi wa wanafunzi, na matokeo ya chuo na kazi kwa wanafunzi wa Ohio wanaozungumza lugha nyingi. Rasilimali ziliundwa kupitia juhudi za kushirikiana kati ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce) na Kituo cha Chuo Kikuu cha Jimbo la Ohio cha Elimu na Mafunzo ya Kazi (The Ohio State University's Center on Education and Training for Employment) pamoja na kikundi cha kujitolea cha watetezi wa familia, viongozi wa jamii, wafanyakazi wa wilaya ya shule, na walimu.*

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 